## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI AGOSTI, 2024 NA MWELEKEO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2024.

**Dondoo za tathmini ya Agosti, 2024 na mwelekeo wa Septemba, 2024:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Agosti, 2024 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Septemba, 2024 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2024 vipindi vya baridi hadi baridi kali viliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini hususan yale yaliyopo nyanda za juu kusini magharibi na nyanda za juu kaskazini mashariki hasa nyakati za usiku na asubuhi.


ii. Vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa Pwani na maziwa makuu. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya mvua vilijitokeza katika ukanda wa Pwani, kanda ya Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

iii. Katika kipindi cha mwezi Septemba 2024, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini pamoja na ongezeko kiasi la joto katika baadhi ya maeneo. Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo yenye miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini katika hiki cha Septemba, 2024.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI AGOSTI, 2024.

Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2024 hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi iliyoambatana na vipindi vya baridi kiasi hadi baridi kali katika baadhi ya maeneo hususan ya nyanda za juu kusini magharibi na yale yenye miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki hasa nyakati za usiku na asubuhi. Kiwango cha chini zaidi cha joto

cha nyuzi joto 3.5 °C kiliripotiwa katika kituo cha Uyole (Mbeya) mnamo tarehe 5 Agosti, 2024. Aidha, vipindi vya upepo mkali unaofikia kasi ya km 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ukanda wa pwani na maziwa makuu. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya mvua viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, ukanda wa pwani na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kiwango cha juu cha mvua cha milimita 23.7 kiliripotiwa katika kituo cha Bukoba mkoa wa Kagera mnamo tarehe 9 Agosti, 2024.




Kielelezo 1: Viwango vya joto la chini kwa vituo vya Uyole na Igeri kwa mwezi Agosti, 2024

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2024

## 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2024, joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo kubwa la Bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo

wenye unyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea ukanda wa pwani na maeneo ya jirani. Katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki, joto la Bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa hali inayoashiria uwepo wa *La Niña* hafifu katika kipindi cha Septemba, 2024. Aidha. Hali ya joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) inatarajiwa kuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani lililopo katika ncha ya kusini ya Afrika linatarajiwa kuendelea na kupelekea kupunguza kuvuma kwa hewa yenye ubaridi kutoka kusini na hivyo kusababisha vipindi vichache vya baridi zaidi nyakati za usiku katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Pwani.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2024

Kipindi cha mwezi Septemba 2024, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuendelea kuwa na hali ya ukavu na ongezeko kidogo la joto. Hata hivyo, hali ya baridi kiasi hadi baridi kali inatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi hususan nyakati za usiku na asubuhi. Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki na Ziwa Victoria. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 26 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na kati ya nyuzi joto 14 °C na 24 °C katika maeneo ya nchi kavu. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi ikiambatana na vipindi vichache vya mvua katika maeneo ya mwambao wa pwani.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 14 °C. Kwa ujumla hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo ya miinuko inatarajiwa kujitokeza.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 16 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**
Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 16 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko (ikijumuisha mkoa wa Njombe) yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 8 °C. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. Aidha, Kiujumla hali ya ukavu inatarajiwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 12 °C. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

**MATARAJIO KWA MWEZI OKTOBA, 2024**

Katika kipindi cha mwezi  Oktoba, 2024 Mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, hali ya joto inatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo.

**2.3 USHAURI**

Tahadhari za kiafya zichukuliwe ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi hiki, maji na malisho yanapaswa kutumika kwa uangalifu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Septemba, 2024 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz